

**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA
BORA, MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI (MB),
KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA 3 CHA
SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC –
JIJINI ARUSHA, FEBRUARI 08, 2023**

*Mhe. Felician Mtahengerwa; Mkuu wa Wilaya ya Arusha
na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Arusha,*

*Dkt. Laurean Ndumbaro; Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

*Dkt. Musa Kissaka; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
ya Mamlaka ya Serikali Mtandao,*

Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao,

*Mhandisi Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu wa
Mamlaka ya Serikali Mtandao,*

*Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi
Mbalimbali,*

*Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka
Taasisi mbalimbali,*

*Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa
Mamlaka ya Serikali Mtandao,*

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana,

Itifaki imezingatiwa.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutukutanisha hapa leo katika tukio hili muhimu la kikaokazi cha tatu (3) cha Serikali Mtandao.

Kipekee, niwashukuru Viongozi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi mbalimbali, ambao mmejumuiika nasi katika kufanikisha kikao hiki. Ni wazi kuwa, uwepo wenu hapa unadhihirisha jinsi mnavyotambua umuhimu wa Serikali Mtandao na mchango wake katika kuleta maendeleo ya Taifa letu hasa katika kuboresha utendaji kazi katika Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa umma. Niwapongeze na kuwasihi kudumisha mtizamo na ushirikiano huu.

Vilevile, niwashukuru Viongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) nikianza na Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti, pamoja na watumishi wote kwa moyo wao

wa kujitoa na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao na kufanikisha kikao hiki.

Ndugu washiriki;

Mamlaka ya Serikali Mtandao ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019. Taasisi hii imepewa dhamana ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma, pamoja na kuhimiza uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma.

Kuimarika kwa Taasisi hii kunatokana na nia ya dhati ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ya kuhimiza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Taasisi za Umma na utoaji

wa huduma kwa Umma ili kuhakikisha kuwa zinapatikana kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

Ndugu washiriki;

Ikumbukwe kuwa, mnamo tarehe 22 Aprili, 2021 **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, wakati akilihutubia Bunge kwa mara ya kwanza mara baada ya kuapishwa kuliongoza taifa letu alieleza bayana kwamba, Serikali yake itatoa kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA hususan katika masuala ya utafiti na ubunifu kwenye eneo la TEHAMA, kuimarisha usalama wa Mtandao wa Mawasiliano, kuongeza watumiaji wa *internet* kutoka asilimia 43 ya sasa hadi asimilia 80 mwaka 2025, ikiwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa mawasiliano ya simu nchi nzima ili kuwawezesha Watanzania kupata huduma bora na kwa

wakati kupitia mifumo ya TEHAMA iliyosanifiwa na Taasisi za Umma kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wananchi.

Ndugu washiriki;

ili kutimiza azma hiyo ya Mhe. Rais ya kuboresha huduma kwa umma kupitia mifumo ya TEHAMA, nitoe wito kwenu ninyi washiriki kutumia kikao kazi hiki kutoa maoni, ushauri na mapendekezo yatakayoiwezesha Serikali inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao zenye tija, ufanisi na zinazoboresha utoaji wa huduma bora kwa umma pamoja na kutoa mchango katika maendeleo ya taifa letu.

Ndugu washiriki;

Mhe. Rais ameelekeza tuimarisha matumizi TEHAMA ili twende sambamba na dunia katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, ambayo yanaongozwa na TEHAMA kwa kuwa shughuli nyingi duniani ikiwemo za kiuchumi kwa sasa zinafanyika kwa kutumia TEHAMA. Hivyo, niendeleo e-GA kuendelea kufanya tafiti ili kuleta bunifu za Mifumo ya TEHAMA itakayoliwezesha taifa kufanikiwa kuimarisha sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji ili kulipeleka mbele taifa letu kimaendeleo.

Ndugu washiriki;

Kupitia TEHAMA, Dunia hivi sasa imekuwa ni kijiji, hivyo Mamlaka ya Serikali Mtandao inapaswa kujielekeza katika kusimamia matumizi sahihi na salama ya TEHAMA katika Taasisi za Umma. Kwa muktaza huu, Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha utawala wake

imejipanga kuongeza kasi ya kufikisha miundombinu ya Mkongo wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu, hususan katika ngazi za Wilaya, na pia kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi (yaani broadband) kutoka asilimia 45 ya sasa hadi asilimia 80 ifikapo mwaka 2025.

Ndugu washiriki;

Katika Dunia ya Uchumi wa Kidijiti tuliyopo sasa, TEHAMA ni nyenzo wezeshi. Kwa umuhimu huo, Serikali imewekeza na kuweka kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao, kwa kujenga Miundombinu na Mifumo Tumizi na ile ya Kisekta inayosaidia kuboresha ufanisi wa uendeshaji wa shughuli zake na utoaji wa huduma kwa Umma.

Aidha, Imeelezwa hapa katika ripoti, kuwa Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma, imefanikiwa kusanifu, kujenga na kusimamia Mifumo na Miundombinu mbalimbali ya TEHAMA inayolenga kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma.

Vilevile, Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi za Umma iendelee kujenga Mifumo ya kisekta ikiwa ni jitihada za kupunguza urudufu wa Mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma. Hivyo kuondoa uhitaji wa kila Taasisi ya Umma kuwa na Mfumo wake, hususan kwa Taasisi ambazo shughuli zake zinafanana.

Ndugu Washiriki; Miongoni mwa mafanikio ya e-GA katika ujenzi wa Serikali Mtandao ni pamoja na kusanifu, kutengeneza na kusimamia Mifumo Shirikishi na ya Kisekta kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma, ambayo inatumiwa na Taasisi hizo katika utekelezaji wa

shughuli zao za kila siku, kama ilivyoainishwa kwenye ripoti iliyowasilishwa hapa.

Vilevile, Mamlaka imeendelea kusimamia uunganishwaji wa Mifumo ya TEHAMA kwenye Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (*Government Enterprise Service Bus-GovESB*) ili kuiwezesha mifumo hiyo kuwasiliana na kubadilishana taarifa. Hata hivyo, muitikio wa Taasisi za Umma kujiunga na Mfumo huu wa GovESB bado uko chini hivyo, nawaagiza Wakuu wote wa Taasisi za Umma kuhakikisha Taasisi zao zinajiunga kwenye Mfumo huo.

Ndugu washiriki; sote ni mashahidi wa namna ambavyo zoezi la **Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022** lilivyoendeshwa kidijiti na kwa ufanisi mkubwa. Ni zoezi ambalo limekuwa la kihistoria kwa kuwa na mafanikio makubwa. Mafanikio ya zoezi hilo, yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na ushiriki wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

ambayo ilifanya kazi kwa weledi usiku na mchana bila kuchoka kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa na Taarifa zote zinakuwa salama kwa matumizi ya sasa na baadae.

Ndugu Washiriki;

Serikali inajivunia sana mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2012, ambapo hapo awali ilijulikana kama Wakala ya Serikali Mtandao hadi sasa ikiwa Mamlaka. Kwa kipindi chote hicho, e-GA imekuwa ni miongoni mwa Taasisi zinazopaswa kuigwa kutokana na weledi, ubunifu na uzalendo walionao katika kutekeleza majukumu yao kuanzia kwa viongozi hadi watumishi.

Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Umma na Utawala Bora, inaendelea kuhakikisha kuwa inaweka mazingira wezeshi ya kisera na kisheria pamoja na

kuijengea uwezo Mamlaka ya Serikali Mtandao ili iweze kufikia malengo iliyojiwekea.

Ndugu Washiriki;

Nihitimishe kwa kurudia tena kuishukuru na kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuandaa Kikao kazi hiki muhimu. Nawashukuru pia wageni wote waalikwa kwa kuhudhuria kikao hiki muhimu. Ni matumaini yangu kuwa, mtatumia kikao hiki kutoa mawazo muhimu ambayo yatasaidia kuimarisha jitihada za kukuza Serikali Mtandao nchini. Hivyo, niwasihi mshiriki kikamilifu kwa kutoa maoni na michango mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao ili kuendana na kauli mbiu ya kikao kazi hiki isemayo ***“Mifumo Jumuishi ya TEHAMA kwa Utoaji Bora wa Huduma za Umma”*** (Integrated ICT Systems for Effective Public Service Delivery).

Baada ya kusema hayo, sasa natamka rasmi kuwa Kikao Kazi chaTatu (3) cha Serikali Mtandao kimefunguliwa Rasmi.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA